(3) The Minister responsible for finance shall submit to the National Assembly estimates for revenue and expenditure of the Judiciary for approval.”

Passed by the National Assembly on 28<sup>th</sup> March, 2015

THOMAS D. KASHILILAH  
Clerk of the National Assembly

## SHERIA YA BAJETI YA MWAKA, 2015

### MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu*

*Jina*

#### SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

#### SEHEMU YA PILI MUUNDO WA MFUMO WA UCHUMI JUMLA NA BAJETI

4. Misingi ya sera ya bajeti.
5. Malengo ya sera za bajeti.
6. Matarajio ya uchumi jumla wa bajeti.
7. Uratibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

#### SEHEMU YA TATU USIMAMIZI WA MCHAKATO WA BAJETI

8. Majukumu ya Bunge.
9. Kamati ya Bajeti ya Bunge.
10. Mamlaka na kazi ya Waziri.
11. Majukumu ya Waziri anayeshughulikia masuala ya Mpango.
12. Mamlaka na kazi za Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali.
13. Mamlaka na kazi ya Tume ya Mipango.
14. Kamishna wa Bajeti.
15. Kamati ya Kitaifa ya Mpango na bajeti.
16. Kamishna wa Uchambuzi wa Sera.
17. Mamlaka na kazi za Msajili wa Hazina.
18. Mamlaka na kazi ya Afisa Masuuli.

SEHEMU YA NNE  
UANDA AJI NA UIDHINISHWAJI WA BAJETI

19. Hatua za uandaaji wa bajeti.
20. Mpango wa Maendeleo wa Taifa.
21. Mpango na Miongozo ya Bajeti.
22. Bajeti za taasisi za umma.
23. Uwasilishaji wa makadirio ya bajeti.
24. Uwasilishaji wa nyaraka nyingine za bajeti mbele ya Bunge.
25. Bunge kujadili makadirio ya bajeti.
26. Kuidhinishwa kwa bajeti ya Taifa na Bunge.
27. Matumizi ya Serikali yaliyoidhinishwa.
28. Wakati ambapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika.
29. Mwisho wa Matumizi ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha.
30. Muda wa matumizi na kibali.
31. Kuwasilisha viashiria vya Sera ya Bajeti.
32. Kuwasilisha Muswada wa Fedha.
33. Kuzuia idhini.
34. Serikali kukiuka malengo ya kibajeti.
35. Vyanzo vya Mfuko wa Dharura.
36. Waziri kusimamia Mfuko wa Dharura.
37. Matumizi kutoka Mfuko wa Dharura.
38. Bunge kuidhinisha fedha zilizotumika kutoka Mfuko wa Dharura.
39. Taarifa za fedha kuhusu Mfuko wa Dharura.
40. Mapato na uwekezaji.
41. Uhamisho wa fedha.
42. Mapato ya ziada.
43. Kuwasilisha bajeti ya nyongeza.

SEHEMU YA TANO  
UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI  
TAARIFA WA BAJETI

44. Mamlaka ya Matumizi.

45. Idhini ya kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu.
46. Utoaji wa malipo.
47. Utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu.
48. Malipo ya fedha kwa Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mamlaka.
49. Kibali cha Mhasibu Mkuu.
50. Dhana ya miadi.
51. Miadi ya miaka mingi.
52. Mfumo wa udhibiti wa miadi.
53. Mikataba ya Miradi ya Maendeleo.
54. Taarifa za ndani ya mwaka.
55. Taarifa ya matumizi ya miadi.
56. Taarifa za utekelezaji wa miadi.
57. Taarifa za Serikali za robo mwaka.

SEHEMU YA SITA  
USIMAMIZI WA MAPATO

58. Msingi ya usimamizi wa mapato.
59. Majukumu ya ukusanyaji mapato na usimamizi.

SEHEMU YA SABA  
USIMAMIZI WA VIFUNGU VIDOGO VYA SERIKALI NA TAASISI  
NJE YA MFUMO WA BAJETI

60. Usimamizi wa kibajeti na kifedha za serikali za mitaa.
61. Mamlaka ya Waziri kusamehe kodi, ada au tozo.
62. Usimamizi wa kibajeti na kifedha na wa asasi nyingine za Serikali.

SEHEMU YA NANE  
MASHARTI YA JUMLA

63. Kanuni na maelekezo.
64. Kuongeza Kipindi cha muda uliowekwa.
65. Uwajibishaji wa Mamlaka iliyoshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria.
66. Hatua za urekebishaji dhidi ya Serikali na taasisi za umma.
67. Kinga kwa maafisa wa umma.

- 68. Masharti ya kuwa na mamlaka ya juu.
- 69. Masharti ya mpito.

SEHEMU YA TISA  
MAREKEBISHO YATOKANAYO

- 70. Tafsiri.
- 71. Kuongezwa kwa kifungu cha 18A.
- 72. Tafsiri.
- 73. Marekebisho ya kifungu cha 44.
- 74. Tafsiri.
- 75. Marekebisho ya kifungu cha 74.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NO.11 YA 2015

NAKUBALI,  
JAKAYA MRISHO KIKWETE*Rais*11<sup>th</sup> Mei, 2015

**Sheria kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia mchakato wa bajeti ya taifa, kuweka misingi ya sera ya bajeti, Mipango na Miongozo ya Bajeti, mamlaka ya Bunge kuhusiana na bajeti; kuainisha mamlaka na majukumu ya Waziri, Katibu Mkuu, Tume ya Mipango na Kamishna wa Bajeti kuhusiana na uandaaji na upitishwaji wa bajeti ya taifa, matumizi na utoaji fedha; kuainisha uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Dharura, utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu, usimamizi wa mapato, usimamizi wa Serikali na taasisi za umma na kwa ajili ya kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

[.....]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano.

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZIJina na  
tarehe ya  
kuanza  
kutumika

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Bajeti ya mwaka, 2014 na itaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2015.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri	<b>3.</b> Katika Sheria hii, isipokuwa pale ambapo muktadha utahitaji vinginevyo-
Sura 348	“Mhasibu Mkuu wa Serikali” atakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Fedha ya Umma;
Sura 348	“Afisa Masuuli” atakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Fedha ya Umma;
	“Sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha” maana yake ni sheria inayohusu matumizi ya fedha za umma kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya usambazaji wa huduma ndani ya mwaka wa fedha;
	“bajeti” maana yake ni makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka mzima na yanajumuisha misaada kwa Serikali za mitaa ambayo imewasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuidhinishwa;
	“mzunguko wa bajeti” maana yake matukio yanayofuatana yanayoonyesha muda wa utakaotumika katika maandalizi ya bajeti kuanzia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, usimamiaji na utoaji taarifa;
	“taarifa ya utekelezaji” maana yake ni moja kati ya taarifa nyingi ambazo zinawasilishwa Bungeni na waziri chini ya kifungu cha 51;
Sura 2	“mfuko wa dharura” maana kama ilivyotafsiriwa katika Katiba;
	“Katiba” maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
	“kuidhinisha matumizi ya fedha” maana yake ni idhini iliyotolewa na Bunge chini ya Sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha, kuruhusu malipo kufanyika kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina au mfuko wowote wa Serikali ulioanzishwa chini ya sheria yoyote kwa masharti maalum;
	“wakala wa asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti” maana yake idara zinazoendeshwa nje ya bajeti ya Serikali;
	“mwaka wa fedha” maana yeke ni, kuhusiana na:
	(a) Serikali kuu, kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoishia tarehe 30 Juni, ya kila mwaka;
	(b) Serikali za mitaa, ili iliyotafsiriwa kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa;
	(c) mamlaka ya umma au taasisi zingine, kipindi kilichobainishwa ndani ya sheria husika au nyaraka zinazohusiana na mamlaka hiyo au taasisi au kipindi kitakachowekwa na mamlaka yenye mamlaka kwa mamlaka hiyo ya umma au taasisi;



- “Serikali” maana yake ni Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretariati za mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa;
- “Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya fedha;
- “miswada ya fedha” maana yake ni Muswada wa Fedha, muswada wa matumizi au muswada mwingine wowote ambao unaweka utaratibu wa masuala ya kifedha;
- “mwaka wa fedha” maana yake ni, kuhusiana na:
- (a) Serikali kuu, kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoisia tarehe 30 Juni ya kila mwaka; na
  - (b) mamlaka ya umma au taasisi zingine, kipindi kilichobainishwa ndani ya sheria husika au nayaraka zinazohusiana na mamlaka hiyo au taasisi au kipindi kitakachowekwa na mamlaka yenye mamlaka hiyo ya umma au taasisi;
- “misingi ya usimamizi mzuri wa fedha” maana yake ni misingi ya fedha za umma kama ilivyobainishwa katika Sheria ya fedha za Umma na ile iliyorejewa katika kifungu cha 4 cha Sheria hii;
- “Mpango na Miongozo ya Bajeti” maana yake ni mwongozo wa mpango na bajeti iliyorejewa katika sheria hii;
- “mwaka ujao wa fedha” maana yake ni kipindi kinachoanzia tarehe 1 Julai ya mwaka mwingine na kuishia tarehe 30 Juni, ya mwaka unaofuata;
- “Mlipaji Mkuu wa Serikali” maana yake afisa aliyepewa mamlaka ya kusimamia fedha za umma kwa mafiasa masuuli na ambaye kwa mamlaka yake atazingatia maelekezo ya Waziri, atasimamia fedha za umma katika Wizara na Idara za Serikali na kufanya kazi nyinginezo kama itakavyoainishwa katika kanuni.
- “Katibu Mkuu” maana yake ni Katibu Mkuu Hazina;
- “taasisi ya umma” maana yake ni wakala, mamlaka na taasisi zote za umma ikijumuisha mashirika ya umma;
- “fedha za umma” zinajumuisha:
- (a) mapato ya umma ya Jamhuri ya Muungano;
  - (b) amana au fedha yoyote ambayo imetunzwa kwa muda au vinginevyo na afisa kwa nafasi yake ya kifisi, aidha peke yake au kwa pamoja na mtu mwingine, awe afisa au la;

- “jumuiya za kiuchumi za kikanda” zinajumuisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Soko la pamoja la Afrika Mashariki na Kusini wa Afrika na Jumuiya nyinginezo za kiuchumi;
- “sheria ya matumizi ya ziada” maana yake ni sheria yoyote ambayo lengo lake ni kuongeza matumizi kwenye matumizi ambayo yalishaidhinishwa kwenye sheria ya matumizi;
- Sura 370 “Msajili wa Hazina” maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Msajili wa Hazina (kazi na mamlaka).

#### SEHEMU YA PILI

#### MUUNDO WA MFUMO WA UCHUMI JUMLA NA BAJETI

Misingi ya sera za bajeti

- 4.-(1)** Serikali na taasisi za umma, katika malengo ya sera zao, itazingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha.
- (2) Misingi ya usimamizi mzuri wa fedha itajumuisha-
- (a) sera ya kukopa ambayo inahakikisha umma kwamba madeni yake yanahimilika;
  - (b) sera za bajeti ambazo zitasaidia kufanikisha na kudumisha kiwango maalum cha tahadhari ili kuwa katika hali nzuri ya kibajeti siku za usoni;
  - (c) kupunguza athari za kibajeti kwa nchi kwa mujibu wa dhamana za mikopo, wajibu katika pensheni na madeni yasiyolipwa;
  - (d) sera ya mishahara inayohimilika, kuvutia, inayoendana na ukubwa wa uchumi, na inayohakikisha kuwepo kwa wafanyakazi wenye tija;
  - (e) sera izinazohakikisha kuwepo kwa mabadiliko ya wastani katika kiwango na uhakika wa viwango vya kodi;
  - (f) mfumo na bajeti ya Taifa yenye kuzingatia uwazi, uwajibikaji na usimamizi mzuri wa uchumi ma sekta binafsi;
  - (g) vipaumbele katika matumizi yenye tija badala ya matumizi yasiyo na tija katika mgawanyo wa rasilimali na
  - (h) kuzingatia dhana ya mgawanyo wa mamlaka kwa kuhakikisha kwamba Bunge linashirikishwa tu katika usimamizi wa rasilimali za umma kama ilivyobainishwa na Katiba na sheria nyingine yoyote.

(3) Waziri atahakikisha kwamba misingi ya usimamizi mzuri wa fedha inazingatiwa wakati wa kuandaa na kutoa taarifa Bungeni juu ya mambo yote yanayotakiwa kutolewa taarifa chini ya Sheria hii.

(4) Serikali inaweza kutozingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha kama Waziri-

(a) ataeleza sababu za kutozingatia misingi hiyo ikijumuisha mpango wa utekelezaji na kipindi ambacho Serikali itakuwa haizingatii misingi ya usimamizi mzuri wa fedha; na

(b) atawasilisha sababu, mpango wa utekelezaji na kipindi cha kutokuzingatia misingi hiyo mbele ya Bunge kwa ajili ya kupitishwa kabla utekelezaji wa sera ya usimamizi wa fedha.

(5) Ukiukwaji wa malengo ya kibajeti utapimwa na kutolewa maelezo katika Mwongozo wa uandaaji Mpango na Bajeti wa mwaka unaofuata.

Malengo ya sera za bajeti

**5.** Mpango na Bajeti utabainisha malengo ya bajeti kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo-

(a) kuhamasisha uhimilivu wa uhakika wa uchumi jumla na ukuaji wa uchumi shirikishi usiokuwa na mfumuko wa bei;

(b) kuanzisha na kuweka mfumo himilivu wa kibajeti na athari ndogo za deni la Taifa;

(c) kuweka wa ukomo wa kibajeti utakaozuia mapungufu katika masuala ya fedha ikiwemo mikopo;

(d) kuweka kiwango cha kutosha cha akiba ya Taifa kuwezesha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi; na

(e) kuwa na uhimilivu na uhakika katika masuala ya fedha.

Matarajio ya uchumi jumla na bajeti

**6.** Programu bajeti na uundaji wa uchumi jumla unaotumika kwa ajili ya sehemu ya mwaka wa fedha kama nyenzo ya uandaaji wa mfumo wa uchumi jumla pamoja na mpango na bajeti utahusisha-

(a) kutathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na athari zake kwenye uchumi wan chi;

(b) kuandaa makisio ya muda wa kati ya uchumi jumla na matarajio ya mwaka ujao wa fedha;

- (c) kuandaa uchumi jumla wa muda wa kati utakaotumika kwa ajili ya kuandaa mpango na bajeti;
- (d) kuandaa mahitaji yanaohusu uchumi jumla na matarajio ya bajeti kwenye nayraka za mpango na bajeti ya taifa; na
- (e) kubainisha majuku ya waziri kutoa matarajio ya uchumi jumla na bajeti kwa kuzingatia muda wa kati.

Uratibu wa  
Mpango wa  
Maendeleo  
wa Taifa

**7.-(1)** Serikali na Taasisi za Umma zitaandaa bajeti zao za mwaka kwa kuzingatia mpango wa muda wa kati na muda mrefu.

(2) Bajeti itakayoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itajielekeza kwenye kutekeleza mpango wa maendeleo wa taifa.

(3) Wakati wa kuandaa bajeti chini ya kifungu hiki, Serikali na Taasisi za Umma hazotjumuishwa kwenye bajeti zao, mradi wowote ambao haukuorodheshwa kwenye mpango wa maende wa Taifa.

(4) Serikali na Taasisi za Umma zitakahkikisha kwamba-

- (a) mipango ya maendelo iliyoidhinishwa ndiyo pekee inatekelezwa;
- (b) mahitaji ya kifedha ya mpango wa maendelo wa taifa yanarandana na kiwango cha ukomo kilichonyeshwa kwenye mpango wa bajeti iliyoelezwa kwenye sheria hii;
- (c) miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa vipaumbele;
- (d) utaratibu wa kutekeleza bajeti ya maendeleo na matumizi, unaanzishwa;
- (e) utaratibu wa kupitia upya mradi wowote mpya wa maendeleo kabla ya kuanza utekelezaji wake, unaanzishwa;
- (f) miradi ya maendeleo inaidhinishwa na Tume ya Mipango kabla haijajumuishwa kwenye bajeti;
- (g) ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuchangia na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kupitia ubia baina ya sekta binafsi na umma;
- (h) vigezo vya juibua vyanzo vya mapato ya serikali za mitaa, vinawekwa;
- (i) upangaji wa madaraja ya serikali za mitaa kwa jaili ya mipango na ugawaji fedha, unafanyika;

- (j) muda kwa ajili ya kukandaa na kusambaza mpango na bajeti unawekwa; na
- (k) vigezo ambavyo kwayo fedha itagawiwa kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo, vinawekwa.

**SEHEMU YA TATU  
USIMAMIZI WA MCHAKATO WA BAJETI**

Majukumu  
ya Bunge

- 8.**-(1) Bunge litakuwa na majukumu yafuatayo-
- (a) kujielekeza kwa makadirio ya awali na mpango wa uchumi jumla na programs;
  - (b) kujadili na kupitia upya mpango na makisio ya bajeti;
  - (c) kusimamia masuala yote ya kibajeti yanayoingia kwenye mamlaka ya Bunge;
  - (d) kuchambua taarifa za kifedha na nyaraka zingine zilizowasilishwa kwake na kutoa maoni kwa Serikali kuhusu uboreshaji wa usimamizi wa fedha za umma;
  - (e) kushauri Serikali kuhusu sheria ya fedha;
  - (f) kutoa ushauri wa jumla kuhusu mwelekeo wa bajeti kwa usuluhishi wake; na
  - (g) kufanya shughuli yoyote inayohusiana na bajeti ambayo sheria yoyote itaitaka kuifanya.
- (2) Katika kutekeleza majukumu yake, Bunge litazingatia misingi ya usimamizi mzuri wa fedha katika mfumo wa bajeti.

Kamati ya  
Bunge ya  
Bajeti

- 9.**-(1) Kamati ya Bajeti itatekeleza, pamoja na majukumu mengine chini ya Kanuni za Kudumu za Bunge majukumu yafuatayo;
- (a) kujadili na kufanya mapitio ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti pamoja na makadirio ya bajeti na kutoa mapendekezo kwa Bunge;
  - (b) kupitia bajeti ya Serikali na kutoa mapendekezo kwa Bunge;
  - (c) kuchambua makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Ukaguzi wa Taifa, Mahakama na Bunge;
  - (d) kutoa mapendekezo kwa Bunge na Kamati za Bunge za Kudumu kuhusu masuala ya kiujumla ya bajeti;

- (e) kufuatilia masuala yote y bajeti yaliyo chini ya mamlaka ya Bunge kupitia Sheria hii au sheria nyingine na kutoa taarifa kwa Bunge;
  - (f) kufuatilia utekelezaji wa Serikali na Taasisi za Umma ili kuhakikisha zinazingatia misingi ya matumizi ya fedha za umma kama ilivyobainishwa kwenye Sheria ya fedha ya Umma na Sheria hii;
  - (g) kupitia taarifa za kifedha za robo mwaka na nyaraka mbalimbali zitakazowasilishwa Bungeni na kutoa mapendekezo jinsi ya kuboresha usimamizi na uwajibikaji wa fedha za umma;
  - (h) kufanya tafiti mara kwa mara kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali na kutoa mapendekezo kwa Bunge jinsi ya kuboresha;
  - (i) kutekeleza kazi au shughuli nyingine zinazohusu masuala ya bajeti kadri Bunge litakavyoelekeza chini ya Sheria hii au sheria nyingine; na
  - (j) kutekeleza majukumu yoyote yaliyobainishwa chini ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, kuhusu usimamizi wa masuala ya bajeti.
- (2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Ofisi ya Bunge itatoa kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti masuala ya bajeti, fedha na kiuchumi.

Mamlaka na  
kazi za  
Waziri

**10.-**(1) Waziri katika kila mwaka wa fedha ataandaa na kuwasilisha Bungeni-

- (a) makadirio ya mapato; na
  - (b) makadirio ya matumizi na mahitaji ya fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa mwaka huo.
- (2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Waziri atakuwa na wajibu wa-
- (a) kuandaa sera ya uchumi jumla na mpango wa matumizi wa bajeti wa muda wa kati;
  - (b) kudhibiti na kusimamia uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa bajeti, ikijumuisha marekebisho yoyote kwenye bajeti;
  - (c) kuhakikisha kuwa wadau wote wanashirikishwa na kufahamishwa kuhusu maamuzi ya kibajeti katika mpango wa muda wa kati ulioandaliwa na waziri chini ya aya (a);

- (d) kutangaza kwa njia zingine zinazofaa, maendeleo ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo mwaka;
  - (e) kusimamia na kudhibiti fedha za Serikali, michakato ya kibenki na malipo, matarajio ya upatikanaji wa fedha, deni la umma na mali na madeni ya Serikali;
  - (f) kutangaza na kutekeleza uwazi na usimamizi yakinifu wa mapato, matumizi, mali na madeni ya Serikali.
- (3) Waziri kwa kutumia kanuni-
- (a) ataaisha utaratibu wa jinsi, wakati na mahali ambapo umma utashirikishwa katika maandalizi ya bajeti kwa ngazi ya kitaifa; na
  - (b) Kamishna wa Bajeti na Mkaguzi Mkuu wa Ndani watatoa utaratibu wa usimamizi wa bajeti kwa kuhakikisha ushiriki binafsi wa maafisa masuuli katika kazi za kamati za bajeti.

Majukumu ya Waziri anayeshughulikia masuala ya Mpango

**11.** Waziri anayeshughulikia masuala ya Mipango atakuwa na jukumu la-

- (a) kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa;
- (b) atawasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuidhinishwa;
- (c) atawasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa ulioidhinishwa kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge;
- (d) ataratibu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa; na
- (e) kuwasilisha Bunge taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa.

Mamlaka na kazi za Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali

**12.-(1)** Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii na sheria ndogo zitakazotengenezwa chini ya sheria hii atawajibika kwa Waziri.

- (2) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali atahakikisha kwamba-
- (a) maandalizi ya makadirio ya matumizi kwa mwaka yanafanyika kwa umakini na wakati kwa ajili ya kuzingatia na kuidhinishwa na Waziri kwa kuzingatia idhini la Baraza la Mawaziri kabla ya kuwasilishwa bungeni;

- (b) makadirio ya mwaka ya matumizi yanaandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya jumla au mahsusi ya waziri inayoonyesha, kadiri iwezekanavyo, thamani ya fedha na matumizi bora ya rasilimali za Serikali;
- (c) mifuko maalum iliyopo na inayokusudiwa kuanzishwa inapitiwa; na
- (d) mfumo utakaowezesha mifuko maalum kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, unaanzishwa.
- (3) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, kwa kuzingatia maelekezo ya waziri atadhibiti utoaji wa fedha za umma kwa Serikali na taasisi zingine za umma na atafanya kazi zingine zozote zitakazo bainishwa na waziri.
- (4) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali anaweza kuomba taarifa ambayo ni muhimu kwa jili ya kuandaa taarifa yoyote chini ya sheria hii.
- (5) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (4) yatakuwa ya maandishi yanayobainisha masharti na tarehe pamoja na muonekano wa taarifa itakayotolewa na taasisi ya umma ambayo itatakiwa kutii ombi.
- (6) Afisa yeyote wa umma ambaye, bila sababu madhubuti, atashindwa kutoa taarifa iliyoombwa chini ya kifungu hiki anafanya kosa la kinidhamu na atachukuliwa hatua za kinidhamu ambazi zitalingana na mazingira ya kosa.
- (7) Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma kwa taasisi za umma itafanya marejeo ya mapato na matumizi ya taasisi za umma.
- (8) Katika kufanya marejeo hayo mara kwa mara Katibu Mkuu anaweza kuamuru kiasi chochote cha fedha kuingizwa katika bajeti ya taifa.
- (9) Waziri anaweza, kupitia kanuni zilizotangazwa kwenye gazeti la Serikali, kubainisha utaratibu wa kufanya marejeo hayo ya mapato na matumizi ya taasisi za umma.

Mamlaka na  
kazi ya Tume  
ya Mipango.

**13. Mamlaka na kazi za Tume ya Mipango zitakuwa-**

- (a) kutathmini hali ya raslimali za taifa kwa maendeleo na kuishauri Serikali juu ya matumizi sahihi ya raslimali hizo;



- (b) kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Serikali kuhusu mipango na usimamizi wa uchumi;
- (c) kutoa mwongozo wa uandaaji wa Mpango wa Taifa na kufutilia mchakato wa maandalizi wa mipango ya mwaka wa muda mfupi, kati na mrefu.

Kamishna  
wa Bajeti

**14.**-(1) Kutakuwepo na Kamishna wa Bajeti.

(2) Kamishna wa Bajeti kwa maelekezo ya Katibu Mkuu atawajibika kuandaa, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya bajeti.

(3) kamishna wa Bajeti katika kutekeleza majukumu yake atawajibika kwa Katibu Mkuu.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, Kamishna wa Bajeti atakuwa na jukumu la-

- (a) kupitia sera za bajeti na kutoa mwongozo kwenye eneo hilo;
- (b) kuchambua mafungu tofauti ya bajeti wakati wa mchakato wa kuandaa mafungu hayo;
- (c) kusimamia bajeti ya Serikali na taasisi za umma;
- (d) kuandaa taarifa za uhamisho wa fedha;
- (e) kusimamia, kutathmini na kutoa taarifa kuhusu bajeti ya Serikali;
- (f) kusimamia na kujumuisha mpango wa mtiririko wa fedha wenye kuzingatia utekelezaji na utoaji taarifa; na
- (g) kutoa ushauri kuhusu miadi ya Serikali yenye kuhitaji rasilimali fedha na taratibu za kibajeti.

Kamati ya  
Kitaifa ya  
Mpango na  
bajeti

**15.**-(1) Kutakuwepo na Kamati ya Kitaifa ya mpango wa bajeti.

(2) Muundo wa kamati ya kitaifa ya mpango wa bajeti utainishwa na Waziri kupitia kanuni.

(3) Kamati ya kitaifa ya mpango na uchumi itakuwa na jukumu la kuishauri Serikali katika kuandaa Bajeti ya nchi.

(4) Mamlaka na kazi ya kamati ya kitaifa ya mpango na Bajeti yatakuwa:

- (a) kuandaa mpango na bajeti kwa mujibu wa sheria hii;
- (b) kuomba taarifa kwa maandishi kutoka Serikalini na taasisi za umma ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuandaa Mipango na Miongozo ya Bajeti;

Kamishna  
wa  
Uchambuzi  
wa Sera

**16.**-(1) Kutakuwa na Kamishna wa Uchambuzi wa Sera.

(2) katika kutekeleza majukumu yake Kamishna wa Uchambuzi wa Sera atakuwajibika kwa Katibu Mkuu.

(3) majukumu ya Kamishna wa Uchambuzi wa Sera yatakuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu wa kisera kuhusiana na-

- (a) masuala ya kisera kuhusu bajeti, ukusanyaji wa mapato, mgawanyo wa matumizi, vyanzo vya fedha na mahusiano ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa; na
- (b) masuala ya uchumi jumla kuhusu utungaji wa sera na utekelezaji, usimamizi wa kanzidata na utoaji wa taarifa wa vipindi.

Mamlaka na  
kazi ya Msajili  
wa Hazina

**17.** Msajili wa Hazina atakuwa na mamlaka na kazi ya-

- (a) kupitia na kupendekeza au kupitisha mikakati na mipango ya mwaka ya taasisi za umma ambazo ziko chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina kabla ya kuingiza kwenye mpango wa Maendeleo ya Taifa;
- (b) kusimamia mifuko ya uwekezaji wa taasisi za umma;
- (c) kufuatilia na kuhakikisha kwamba ziada, michango na gawio kutoka taasisi za umma zinalipwa kwa wakati;
- (d) kuelekeza au kupitisha, matumizi au marekebisha ya Kanuni za fedha ili kuhakikisha mapato na matumizi ya taasisi za umma;
- (e) kusimamia mitaji, ruzuku, fedha za mitaji, akiba au mapato yaliyosalia, yaliyolipwa na shirika na uwekezaji mwingine wa umma;

- (f) kuchambua na kuidhinisha muundo wa taasisi, muundo wa mishahara, kada za utumishi katika taasisi za umma;
- (g) kusimamia fedha zilizopokelewa kutokana na ubinafsishaji wa taasisi za umma, mali na hisa;
- (h) kufanya mapitio na kusaini mikataba ya utekelezaji ya mashirika ya umma yenye lengo y kuboresha mapato; na

Mamlaka na  
kazi ya  
Maafisa  
Masuuli

**18.(1)-Mamlaka na kazi za Maafisa Masuuli zitakuwa ni kuhakikisha kwamba-**

- (a) mafungu ya bajeti na taasisi za umma zinaandaliwa kwa mujibu wa Miongozo na Miongozo ya Bajeti;
- (b) fedha za umma na rasilimali za umma zinalindwa na kusimamiwa ipasavyo; na
- (c) kuna mpangilio mzuri wa kuwezesha kukusanya mapato kutoka kwa umma.

(2) Maafisa Masuuli wa Wizara na taasisi za umma wataanzisha kamati za bajeti ambazo muundo wake utainishwa katika kanuni.

#### SEHEMU YA NNE UANDAAJI NA UIDHINISHWAJI WA BAJETI

Hatua za  
uandaaji wa  
bajeti

**19.-(1) Matayarisho ya Bajeti kwa kila mwaka wa fedha yatahusisha hatua zifuatazo-**

- (a) majumuisho ya mchakato wa mipango ya maendeleo ambayo itakuwa ile mipango ya muda mrefu na muda wa kati;
- (b) mipango na maamuzi ya sera za kifedha na kiuchumi pamoja na vipaumbele vya ngazi ya kitaifa kwa muda wa kati;
- (c) Baraza la Mawaziri kuidhinisha Mwongozo wa Mpango wa Bajeti;
- (d) Bunge kuidhinisha Mwongozo wa Bajeti na Mpango kama msingi wa maamuzi ya kuandaa makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaofatia;
- (e) Baraza la Mawaziri kuidhinisha hatua na vyanzo vya mapato;
- (f) Bunge kuidhinisha hatua na vyanzo vya mapato;

- (g) kuwasilisha makadirio ya bajeti Bungeni kwa ajili ya kupata kibali;
  - (h) kuandaa Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali, Muswada wa Sheria ya Fedha na Sheria nyingine zinazohitajika kutungwa kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali;
  - (i) kutunga Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali na Sheria ya Fedha;
  - (j) kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa;
  - (k) kufanya tathmini na kutoa taarifa za mapato na matumizi ya bajeti ya Serikali; na
  - (l) kufanya mapitio na kutoa taarifa kuhusu mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu.
- (2) Kutakuwa na kamati ya kumshauri Waziri kuhusu vyanzo vya mapato katika mwaka wa fedha husika.
- (3) Muundo wa kamati ya hiyo ya ushauri utaainishwa na Waziri katika kanuni.

Mpango wa  
Maendeleo wa  
Taifa

**20.** Waziri anayeshughulikia Tume ya Mipango ataandaa na kuwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambao utakuwa msingi wa uandaaji wa bajeti ya Taifa.

Mpango na  
Mwongozo wa  
Bajeti

**21.**-(1) Waziri ataandaa na kuwasilisha Bungeni Mpango na Mwongozo wa Bajeti.

(2) Mpango na Mwongozo wa Bajeti utawasilishwa Bungeni kila Februari ya kila mwaka, au pale ambapo Bunge halitakuwepo mwezi Februari, kila wiki ya kwanza Bunge litakapokutana.

(3) Mpango na Miongozo ya Bajeti utaeleza kwa mapana malengo ya masula ya Uchumi Jumla ambayo yatakuwa msingi wa bajeti kwa kipindi kinachofuata mwaka wa fedha uliopo na mipango ya kati na itazingatia yafuatayo-

- (a) tathimini ya mwaka wa fedha uliopo na uchumi unaotarajiwa kwa miaka ya fedha mitatu inayofuata;

- (b) uchumi jumla na sera za kibajeti kwa kipindi kilichobainishwa chini ya aya (a);
  - (c) malengo ya mapato kwa ujumla, matumizi kwa ujumla, ukopaji wa ndani nan je kwa kipindi kinachofuata mwaka wa fedha na mipango ya kati;
  - (d) jumla ya rasilimali zilizogawanywa kwa ajili miradi ya kissekta au Wizara kwa kipindi kilichobainishwa chini ya aya (a) ilibainisha matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa kila mradi kwa kipindi hicho;
  - (e) vigezo vilivyotumika kugawa rasilimali za umma zilizopo kwa kila mradi;
  - (f) makadirio ya riba na gharama za ulipaji madeni na ulipaji wa madeni kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa bajeti husika na miaka miwili ya fedha inayofuata;
  - (g) mapendekezo ya kugharimia mapungufu yoyote kwa mwaka wa fedha;
  - (h) makusudio kuhusu ukopeshaji na vitu vitakavyosababisha kuongezeka kwa deni ya Taifa kwa mwaka wa fedha;
  - (i) bajeti na hali halisi ya mapato kwa miaka miwili ya fedha iliyotangulia;
  - (j) bajeti na hali halisi ya matumizi kwa miaka miwili ya fedha iliyotangulia kwa kila fungu na Idara muhimu;
  - (k) makadirio ya hali ya kifedha kwa mwaka wa fedha unaohusika na bajeti na miaka miwili inayofuata;
  - (l) malengo ya kisera yanayosimamia maamuzi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha na maeneno ya kisera ambayo Serikali itazingatia katika mwaka wa fedha.
- (4) Kamati ya Bunge ya Bajeti kabla ya kumalizika kwa siku saba baada ya kuwasilishwa kwa Mwongozo wa Mpango na Bajeti Bungeni, itawasilisha taarifa yenye mapendekezo ambapo Bunge litayajadili na kupitisha azimio kukubali bila marekebisho au na marekebisho.

(5) Waziri ataitisha na kusambaza Mwongozo wa Mpango na Bajeti ndani ya siku zisizozidi kumi na tano baada ya kuwasilishwa Bungeni.

Bajeti za  
taasisi za  
umma

**22.**-(1) Taasisi za Umma zitatakiwa kuandaa makadirio ya bajeti na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya uchambuzi na idhini kwa mujibu wa Sheria hii na kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.

(2) baada ya kupokea makadirio ya bajeti, katibu mkuu anaweza:

(a) kuidhinisha makadirio ya bajeti yakiwa na mabadiliko au bila mabadiliko;

(b) kukataa makadirio ya bajeti na kutoa sababu za kukataa;

(3) Katibu Mkuu anaweza kufanya mabadaliko au kukataa makadirio ya bajeti kwa misingi ya sababu mahsusi zilizotajwa kama zinazoainishwa-

(a) makadirio hayaangukii katika majukumu ya msingi ya taasisi za umma husika;

(b) makadirio hayo ni ya juu zaidi na hayalingani na mahitaji halisi ya utoaji au upokeaji wa huduma katika soko au

(c) hayaendani na hatua za kubana matumizi zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa.

(4) Katibu Mkuu anaweza, kuamuru mapato yaziada ya bajeti yaliyokusanywa na taasisi za umma kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu .

Uwasilishaji  
wa makadilio  
ya bajeti

**23.**-(1) Waziri atatakiwa, ndani ya kipindi kilichowekwa na kubainishwa katika kifungu hiki, kuwasilisha kwa Baraza la Mawaziri kupata kibali cha makadirio ya bajeti na nyaraka nyinginezo zitakazozingatwa katika makadirio ya bajeti.

(2) Endapo Baraza la Mawaziri litakapokuwa limetoa kibali kwa makadirio ya bajeti kwa mujibu wa kifungu kidogo (1), Mawaziri wote watatakiwa kuwa na jukumu la:

(a) kuzingatia, kufuata na kusimamia makadilio ya bajeti;

(b) kusimamia utekelezaji wa makadirio ya bajeti

(3) Waziri atatakiwa, ndani ya kipindi kilichobainishwa katika Kanuni za Bunge kuwasilisha Bungeni nyaraka zifuatazo-

- (a) makadirio ya bajeti;
- (b) nyaraka zinazohusiana na makadirio ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti.

(4) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), Serikali itahakikisha kuwa Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama umepewa fedha za kutosha kuwezesha Bunge na Mahakama kutekeleza kazi na majukumu yake kwa ufanisi.

(5) Serikali na Bunge .

(6) Waziri atatangaza baada ya kuwasilisha Bungeni Makadirio ya bajeti na nyaraka zinazohusiana na makadirio ya bajeti katika Gazeti la Serikali na kuzisambaza kwa umma.

(7) Waziri ataandaa mara baada ya kupata idhini ya bunge kuhusu makadirio ya bajeti, kuwasilisha Bungeni Muswadawa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa makadirio yaliyoidhinishwa.

Uwasilishaji  
wa nyaraka  
**nyingineza**  
bajeti mbele ya  
Bunge

**24.**-(1) Pamoja na nyaraka zilizowasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 22, Waziri atapaswa kuwasilisha Bungeni nyaraka za bajeti kwa kila mwaka wa fedha-

(a) muhtasari wa bajeti unaojumuisha:

- (i) muhtasari wa sera za kibajeti zinazojumuisha sera za mapato, matumizi, madeni na upungufu wa fedha;
- (ii) maelezo ya jinsi bajeti inavyohusika na misingi ya wajibu wa kibajeti na malengo ya kibajeti na
- (iii) maelezo ya Waziri kuhusu makubaliano ya Bunge kwenye Mpango na Miongozo ya bajeti ilivyoshughulikiwa;
- (iv) mgao wa mapato kwa serikali za mitaa kutoka hisa za Serikali ikiwemo misaada yenye masharti na isiyo na masharti;

(b) muundo wa makadirio ya bajeti yanayojumuisha:

- (i) orodha ya taasisi zote zinazopata fedha kutoka bajeti ya Serikali;

- (ii) makadirio yote ya mapato kwa wigo mkubwa wa uchumi;
- (iii) makadirio yote ya matumizi, mafungu ya miradi, ikibainisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo; na
- (iv) makadirio ya mapungufu ya bajeti au ongekezo kwa mwaka wa fedha na mipango ya kati na mapendekezo ya vyanzo vya fedha;
- (c) taarifa kuhusu madeni yatokanayo na bajeti ya Serikali, inayojumuisha makadirio ya deni, riba na gharama zinginezo zinazotakiwa kulipwa na Serikali katika mwaka wa fedha kwa mujibu wa madeni husika;
- (d) taarifa kuhusu madeni na dhamana za Serikali, yanayojumuisha makadirio ya deni, riba na gharama zinginezo zinazotakiwa kulipwa na Serikali katika mwaka wa fedha kwa mujibu wa madeni husika;
- (e) taarifa kuhusu malipo yatakayolipwa na gharama zitakazolipwa na Serikali ambazo hazikubainishwa katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali ambazo zinajumuisha masuala ya kikatiba na mamlaka ya Sheria kufanya malipo hayo na
- (f) taarifa ya Waziri kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Bunge kuhusu bajeti ya Serikali katika mwaka au miaka iliyopita.
- (2) Waziri atatoa ufafanuzi wa taarifa zitakazowasilishwa pamoja na makadirio ya bajeti na mfumo wa uwasilishwaji utakaotumika.

Bunge kujadili  
makadirio ya  
Bajeti

**25.**-(1) Kable ya Bunge kujadili makadirio ya bajeti, Kamati ya Bunge itajadili makadirio hayo na kuwasilisha mapendekezo Bungeni kwa kuzingatia maoni ya Waziri na umma yaliyowasilishwa kabla ya tarehe ya mwisho itakayobainishwa katika Kanuni.

(2) Kwa kuzingatia masharti yaliyobainishwa katika Katiba, Bunge linaweza kurekebisha makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Azimio litakalopitishwa kuhusu Mwongozo wa Mpango wa Bajeti kwa kuhakikisha kwamba-



- (a) ongezeko la matumizi katika kasma pendekezwa linawianisha kwa punguzo la matumizi kwenye kasma nyingine;na
- (b) pendekezo la kupunguza matumizi linatumika kupunguza nakisi ya bajeti.

Kuidhinishwa  
kwa Bajeti ya  
Taifa na  
Bunge

**26.**-(1) Bunge litaidhinisha ifikapo tarehe 30 Juni kila mwaka, bajeti ya Taifa pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata na kupitisha Muswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali, Muswada wa Fedha na hati nyingine za kisheria ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa bajeti ya Taifa.

(2) Bunge litaidhinisha bajeti ya Taifa ya mwaka kwa kupiga kura kwa kuita jina kwa kila mbunge.

Matumizi ya  
Serikali  
yaliyoidhinish  
wa

**27.**-(1) Waziri wa Fedha atahakikisha kuwa matumizi yatakayoidhinishwa katika makadirio ya bajeti katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali yanawasilishwa yakiwa-

- (a) sahihi na zimezingatia masuala muhimu ya kibajeti; na
- (b) yamebainisha wazi fedha zilizopo katika fungu na miradi.
- (2) Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali itajumuisha-
  - (a) matumizi ya kawaida kwa kila mradi, ikiainisha kila matumizi husika; na
  - (b) matumizi ya maendeleo kwa kila mradi wa maendeleo, ikiainisha kila matumizi husika.
- (3) Makadirio ya bajeti yaliyoidhinishwa na Bunge yatachukuliwa kuwa kama yameidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za Serikali na Taasisi za Umma.
- (4) Fedha zilizoidhinisha kwa matumizi ya Serikali na taasisi za umma, zitatumika kwa kuzingatia madhumuni yaliyoainishwa na katika kiwango kilichowekwa kwa makadirio ya Serikali na taasisi za umma.
- (5) Waziri katika kipindi cha siku thelathini baada ya Bunge kuidhinisha makadirio ya bajeti, ataboresha, atachapisha na kutangaza kwa umma makadirio ya bajeti.

(6) Waziri atahakikisha na kuchukua hatua kuhakikisha makadirio yaliyoidhinishwa yametayarishwa na kutangazwa katika muundo ambao utakuwa wazi na rahisi kueleweka na kupatikana kwa umma.

Wakati ambapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika

**28.**-(1) Endapo Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali haijaanza kutumika, Rais anaweza kwa kutumia Warrant iliyosainiwa na resident iliyoelekezwa kwa Waziri, akaruhusu matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuwezesha kazi za Serikali kuendelea mpaka tarehe 31 Oktoba ya mwaka wa fedha husika au kwa kuanza kutumika kwa Sheria hii, chochote kitakachotangulia.

(2) Kiasi kitakachoruhusiwa kutumika hakitakiwi kuzidi kiasi kilichoainishwa kwa ajili ya mapendekezo ya shughuli zilizokadiwa kwa mwaka wa fedha au moja ya tatu ya kiasi kilichoainishwa katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali.

(3) Fedha zilizotumika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) kitahesabiwa kama sehemu ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha katika Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali inayohusishwa.

Mwisho wa Matumizi ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha

**29.**-(1) Fedha ambazo hazijatumika kufikia mwisho wa mwaka ambazo ziliidhinishwa matumizi yake yataishia mwaka huo wa fedha.

(2) Kwa kuzingatia sheria zingine, endapo mwisho wa mwaka wa fedha taasisi za umma bado ina bakaa ya fedha zilizoidhinishwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, fedha hizo zitarudishwa kwenye Mfuko Mkuu wa hazina, taasisi ya umma itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Kamishna wa Bajeti.

(3) Kifungu kidogo cha (2) hakitatumika kwa fedha zilizoidhinishwa kuvuka mwaka wa fedha kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

(4) Mhasibu Mkuu wa Serikali atazijumuisha taarifa zilizowasilishwa kwao kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) na kuziwasilisha kwa Waziri taarifa ya fedha ambazo hazikutumika na kuhifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

(5) Waziri wa Fedha atalazimika, kila mwisho wa mwaka wa fedha, kuwasilisha Bungeni taarifa ya fedha ambazo hazikutumika na kuhifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na pendekezo la Serikali ya kutumia hizo fedha katika mwaka mwingine wa fedha ili kupata idhini ya Bunge.

Muda wa matumizi na kibali

**30.**-(1) Matumizi yote ya fedha za umma yaliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya huduma za mwaka wa fedha na kila kibali na idhini nyingine zilizotolewa na sheria hii kuhusiana na mwaka husika, itaisha na kukoma kuwa na nguvu inapofika mwisho wa mwaka wa fedha.

(2) Fedha zote ambazo hazijatumika na ambazo zilitolewa kwenye Mfuko Mkuu zitarejeshwa kwenye Mfuko Mkuu.

Kuwasilisha viashiria vya Sera ya Bajeti

**31.**-(1) Waziri, katika kila mwaka wa fedha baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, atatangaza kwa umma viashiria vya sera za bajeti pamoja na hatua za kukusanya mapato ya Serikali.

(2) Wakati akitoa tangazo hili, atazingatia makubalino ya kikanda na kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeingia, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Afrika Mashariki mwaka 1994 na pale ambapo mikataba hiyo inahitaji kutangazwa kwa hatua hizi katika tarehe maalum, Waziri atahakikisha hatua hizi zinatangazwa katika tarehe husika.

Kuwasilisha Muswada wa Fedha

**32.**-(1) Waziri ataandaa na kuwasilisha Bungeni, Muswada wa Fedha akiainisha hatua za kuongeza mapato ya Serikali.

(2) Katika kuwasilisha Muswada wa Fedha, Bunge litawasilisha mapendekezo yake kuhusu Muswada wa Fedha.

(3) Mapendekezo yote yatakayotolewa na Bunge au kuchukuliwa na Bunge katika masuala ya mapato yata-

(a) zingatia kwamba kiwango cha mapato kitakachokusanywa kinaendana na misingi ya bajeti iliyoidhinishwa;

(b) kuzingatia misingi ya usawa, uhakika na wepesi wa kukusanya;

- (c) kuzingatia athari za mapendekezo ya mabadiliko katika mchanganuo wa kodi kwa kuzingatia kodi ya moja kwa moja na kodi inayoingizwa kwenye bidhaa;
  - (d) kuzingatia mwenendo wa mapato ya ndani, kanda na kimataifa;
  - (e) kuzingatia athari katika maendeleo, uwekezaji, kukua kwa uchumi; na
  - (f) kuzingatia kodi na makubaliano mengine ya viwango na majukumu ambayo Jamhuri ya Muungano imechukuwa, ikiwa ni pamoja na kodi na makubaliano ya viwango katika makubaliano ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 1994.
- (4) Mapendekezo yatakayotolewa chini ya kifungu hiki yatazingatia misingi ya usimamizi wa mapato.

Kuzuia idhini

**33.**-(1) Pale ambapo Bunge limeridhika kuwa zipo sababu za kutosha zilizopelekea kushindwa kutekeleza kwa mapendekezo ya ukaguzi uliopita yaliyofanywa na Bunge, Bunge linaweza kuzuia matumizi ya kifungu maalum ndani ya Fungu, kutoka Mfuko Mkuu, kama takavyoona inafaa kwa madhumuni ya kugharamia matumizi ya Fungu hilo.

(2) Pale ambapo kwa hiari, Fungu hilo limekuwa kwa mfululizo likishindwa kutekeleza au kujibu hoja za ukaguzi na mapendekezo, Bunge linaweza, kwa mujibu wa taratibu za haraka utakavyoona inafaa, kuzuia fedha hizo kutoka katika Fungu hilo kwa mwaka kulingana na kiasi cha fedha kilichohojiwa kuhusu Fungu hilo.

(3) Pale ambapo Bunge limeridhika kuwa kwa hiari na mfululizo Fungu limeshindwa-

- (a) kuzingatia misingi ya umakini na usimamizi mzuri wa fedha;
- (b) kuzingatia misingi bora ya uhasibu na usimamizi wa fedha; au
- (c) kufikia malengo na madhumuni ya bajeti linaweza, pamoja na taratibu nyingine itakavyoona ni za haraka, kuzuia kifungu kimoja au zaidi katika fundu kwa huduma mbalimbali katika Fungu hilo.

(4) Kutokana na kushindwa kwa mfululizo kwa Idara katika seksheni hii ambao unatokana na utendaji mbaya wa Afisa wa Umma, Bunge linaweza, kwa kura ya wachache, na kwa kuzingatia masharti kama itakavyoona inafaa, kuzuia mafano yoyote na mshahara wa Afisa huyo kwa muda itakavyoona inafaa.

(5) Pale ambapo Fungu linawasilisha mbele ya Bunge kuonesha kuwa limeyafanyia kazi mapendekezo ya ukaguzi wa hesabu, Bunge linaweza, iwapo sheria ya Fedha haijaidhinishwa, kuidhinisha malipo ya Fungu hilo kwa namna itakavyoona inafaa.

(6) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza, katika taarifa yake kwa Bunge, kupendekeza kuzuia matumizi ya kifungu chochote katika seksheni hii.

(7) Katika kifungu hii-

- (a) 'kuzuia' ina maana kuzuia, kiasi Fulani au kiasi chote, kwa muda mfupi au moja kwa moja, kifungu kimoja au zaidi ambacho kipo katika makadirio ya mwaka; na
- (b) fungu, linajumuisha Wizara au Taasisi ya Umma.

Serikali  
kukiuka  
malengo ya  
kibajeti

**34.**-(1) Serikali inaweza, kwa idhini ya Bunge, kukiuka malengo ya kibajeti kutoka katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa muda mfupi pale ambapo ukiukaji huu unatokana na majanga ya asili au tukio lingine jingine ambalo halikutarajiwa kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 35.

(2) Pale ambapo yapo mabadiliko ya Serikali, Serikali mpya inaweza, kwa idhini ya Bunge, kukiuka malengo ya kibajeti katika Mwongozo wa Mpango wa Bajeti bila ya kukiuka misingi ya bajeti.

(3) Waziri atawasilisha bungeni taarifa ya ukiukaji wa malengo ya bajeti, na atajumuisha katika taarifa hiyo-

- (a) sababu na matokeo ya ukiukaji huo;
- (b) mapendekezo ya kushughulikia uhamisho huo;
- (c) muda unaokisiwa wa mabadiliko haya; na
- (d) hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na Serikali na iwapo kuna mradi uliosimamishwa, na sababu za kufanya hivyo.

(4) Waziri atalazimika, ndani ya kipindi cha siku thelathini baada ya kuwasilisha Bungeni, kutangaza na kusambaza taarifa zilizowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (3).

Vyanzo vya  
Mfuko wa  
Dharura

**35.**-(1) Mfuko wa Dharura ulioanzishwa utajumuisha fedha zilizotengwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Sheria ya Fedha katika kila mwaka wa fedha.

(2) Mfuko wa Dharura utakuwa ni sehemu ya bajeti ya Serikali na Bunge linaweza kuidhinisha fedha itakavyoona inafaa kwa ajili ya kutunisha Mfuko huo.

(3) Mfuko wa Dharura utakuwa sehemu ya Bajeti ya mwaka na Bunge, pamoja na viwango vilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (2), litaidhinisha fedha nyingine kwa kadri litakavyoona inafaa.

Sura 418

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi, atatoa taarifa katika Bunge kuhusu hesabu za Mfuko wa Dharura.

Waziri  
kusimamia  
Mfuko wa  
Dharura

**36.**-(1) Waziri atasimamia Mfuko wa Dharura.

(2) Kiwango cha Kudumu cha Mfuko wa Dharura hakitazidi kiwango kilichoelezwa na Waziri baada ya kuidhinishwa na Bunge.

(3) Waziri atatumiza Mfuko wa Dharura katika akaunti tofauti, katika Benki Kuu ya Tanzania na-

(a) atafanya malipo kwenye akaunti ya mfuko wa dharura kutoka kwenye mfuko wa Serikali kupitia sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha; na

(b) atalipa kutoka mfuko wa dharura bila kuchelewa, matumizi yote kwa mujibu wa kifungu cha 35.

Matumizi  
kutoka Mfuko  
wa Dharura

**37.**-(1) Waziri anaweza kutoa fedha kutoka Mfuko wa Dharura pale ambapo, kwa msingi wa vigezo vilivyowekwa na mfumo na taratibu za mwongozo wa uendeshaji zilizotajwa na kuidhinishwa na Bunge pamoja na sheria kuhusiana na kudhibiti majanga akiridhika kuwa ipo dharura na jambo lisilotarajiwa na kusababisha umuhimu wa kufanya matumizi ambayo hayamo katika sheria yoyote maalum.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Waziri kwa kuongozwa na Sheria na Kanuni zilizopo, amethibitisha kuwa-

(a) malipo hayakukasimiwa katika bajeti kwa sababu hayakutarajiwa na hayawezi kusubiri mpaka mwaka ujao wa fedha bila kuathiri manufaa kwa umma; na

(b) tukio halikutegemewa.

(3) Pamoja na Kanuni na Sheria husika, kwa madhumuni ya Seksheni hii, tukio lisilotegemewa ni lile ambalo-

(a) linatishia kwa kiasi kikubwa uhai na ustawi wa binadamu;

(b) linatishia uharibifu mkubwa wa mazingira; na

(c) linahusisha kuokoa uharibifu, hasara, ugumu, mateso yanayosababishwa moja kwa moja na tukio hilo.

(4) Tukio litachukuliwa kwamba linatishia uhai wa binadamu au ustawi pale tu linapohusisha, kusababisha au linaweza kusababisha-

(a) kupotea kwa uhai, ugonjwa wa binadamu au maumivu;

(b) kukosa makazi au uharibifu wa mali;

(c) kuharibika kwa chakula, maji na makazi.

(5) Fedha katika Mfuko wa Dharura zinatunzwa kwa matumizi ya majanga ya asili zinaweza kutumika kumuokoa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameathiriwa na majanga ya asili yaliyotokea nje ya Jamhuri ya Muungano, pale ambapo masharti ya kifungu kidogo cha (1) yamezingatiwa.

(6) Mchango wa fedha kwenda katika Fungu, kuhusu majanga ya asili, utatangazwa na Waziri ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa.

(7) Kwa kuzingatia kifungu kidogo (2), Waziri, kwa mujibu wa kanuni na idhini ya Bunge, ataweka vigezo vya kutoa fedha kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

Bunge  
kuidhinisha  
fedha  
zilizotumika  
kutoka Mfuko  
wa Dharura

**38.**-(1) Waziri, ndani ya miezi miwili baada ya kufanya malipo kutoka Mfuko wa Dharura atawasilisha Bungeni taarifa ya kina kuhusu malipo yaliyofanyika akizingatia mahitaji ya taarifa yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha 37(2) na kupata idhini ya Bunge kuhusu malipo hayo.

(2) Pale ambapo Bunge halikutani katika kipindi kilichotajwa katika kifungu kidogo (1), au halitakutana katika mwisho wa kipindi hicho na Waziri hajaomba idhini ya Bunge kabla ya kipindi hicho kuisha. Waziri ataomba idhini hiyo ndani ya siku kimi na tano baada ya Bunge lijalo kuketi.

(3) Mara tu baada ya Bunge kuidhinisha malipo, Waziri atawasilisha Muswada wa Fedha kupelekwa Bungeni kupata idhini ya fedha zilizotolewa ziweze kurudishwa katika Mfuko wa Dharura kwa kiasi kilichotumika.

Taarifa za  
fedha kuhusu  
Mfuko wa  
Dharura

**39.**-(1) Waziri, ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa za fedha za mwaka huo kuhusiana na Mfuko wa Dharura.

(2) Waziri atajumuisha taarifa zifuatazo katika taarifa za fedha zinazoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

- (a) tarehe na kiasi cha kila malipo yaliyofanyika kutoka Mfuko wa Dharura;
- (b) mtu ambaye kwake malipo yamefanyika;
- (c) madhumuni ya kufanya malipo hayo;
- (d) iwapo mtu ambaye malipo yamefanyika kwake ametumia fedha hizo kwa madhumuni hayo, taarifa kuhusu hilo;
- (e) iwapo mtu ambaye malipo yamefanyika kwake, bado hajatumia fedha hizo kwa madhumuni hayo, taarifa kuhusu sababu za kutofanya hivyo; na
- (f) taarifa ya kuonesha ni kwa namna gani malipo yamezingatia vigezo vya kufanya malipo hayo.

Mapato na  
Uwekezaji

**40.** Fedha hazitaingia katika Mfuko wa Dharura isipokuwa zile ambazo zimeidhinishwa kwa Sheria ya Bunge pamoja na riba au mapato mengine ambayo yanaweza yakaingizwa katika Mfuko wa Dharura na fedha hizo zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.



Uhamisho wa  
Fedha

**41.-**(1) Afisa Masuuli anaweza, baada ya kupata idhini ya Waziri, atahamisha fedha kutoka matumizi yaliyoidhinishwa.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo (1), Afisa Masuuli hatafanya uhamisho wa fedha pale ambapo-

- (a) Fedha hizo zimeidhinishwa kwa ajili ya yaliyozuiwa kwa matumizi ya shughuli maalum;
- (b) Fedha hizo zimeidhinishwa kwa ya ofisi nyingine ya Serikali au mtu;
- (c) fedha zimeidhinishwa kwa matumizi ya uwekezaji to defray matumizi mengine ya maendeleo;
- (d) uhamisho wa fedha ni kutoka katika mishahara kwenda katika matumizi yasiyo ya mishahara; au
- (e) uhamisho wa fedha unaweza kusababisha kuvuruga misingi ya bajeti.

(3) Afisa Masuuli anaweza kufanya uhamisho wa fedha za miradi kati ya mafungu katika bajeti ya mwaka wa fedha, iwapo-

- (a) vipo vifungu katika bajeti za miradi ya mafungu ambavyo vinaweza visitumike;
- (b) maombi ya uhamisho wa fedha yamewasilisha hazina yakitoa maelezo ya ufafanuzi kuhusu uhamisho wa fedha na Hazina imeidhinisha maombi hayo; na
- (c) Kiwango cha jumla cha uhamisho wa fedha kulikofanywa kwenda au kutoka katika miradi au mafungu kwa kiwango kisichozidi matumizi yaliyoidhinishwa katika mradi huo au mafungu katika mwaka huo wa fedha.

(4) Waziri anaweza, kwa kanuni, kuidhinisha uhamisho wa fedha ndani ya bajeti za mafungu yaliyoidhinishwa na uhamisho wa fedha ndani ya mafungu au miradi.

(5) Mamlaka ya Waziri katika uhamisho wa fedha katika bajeti hayatekelezwa-

- (a) kiwango cha fedha katika mafungu tofauti;
- (b) kutoka matumizi ya maendeleo kwenda matumizi ya kawaida. Isipokuwa, uhamisho umeidhinishwa kwa bajeti ya nyongeza, na hauzidi kiwango kilichoidhinishwa katika Fungu.

(6) Afisa Masuuli anaweza kuhamisha fedha za ndani ya Fungu bila ya kupata idhini ya Waziri kwa kiwango cha asilimia kilichoidhinishwa katika kanuni na kutoa taarifa kwa Malipaji Mkuu wa Serikali katika kila robo ya mwaka kuhusu uhamisho huo.

(7) Uhamisho wowote wa fedha:-

- (a) utafanyika kwa kushauriana na Wizara zote zilizoathirika pamoja na Taasisi za Serikali; na
- (b) utawasilishwa Bungeni na kutolewa taarifa kila robo mwaka.

Mapato ya ziada

**42.**-(1) Mapato yote yaliyokusanywa zaidi ya kiwango kilichotajwa katika makadirio kitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(2) Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Fedha za Umaa, taarifa ya matumizi ya ziada itakatakatishwa na taarifa ya Afisa Masuuli husika ikielezea sababu na matumizi ya ziada na hatua za kuchukua kuzuia matumizi hayo ya ziada yasitokee.

Kuwasilisha bajeti ya nyongeza

**43.**-(1) Serikali itawasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa.

(2) Bajeti ya Nyongeza itahitajika kwa-

- (a) kuongeza au kupunguza katika idhini mabadiliko ya malengo, au kupata idhini mpya katika sheria ya fedha.
- (b) kuongeza au kupunguza kiwango cha line item katika makadirio iwapo hayataweza kufikiwa katika mabadiliko ya fedha au mabadiliko ya matumizi yake.
- (c) kuonesha namna ambayo Mfuko wa Dharura umetumika.

(3) Endapo Bunge limeidhinisha matumizi, Sheria ya Fedha itapitishwa kwa kiwango kilichoidhinishwa.

(4) Bajeti ya Nyongeza itajumuisha taarifa ya matumizi ya ziada na mapato husika katika kipindi hicho katika kutekeleza misingi ya fedha na Bajeti.

## SEHEMU YA TANO

## UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA WA BAJETI

Mamlaka ya  
Matumizi

**44.** Mahali ambapo Serikali na taasisi na mashirika ya umma yanakuwa na matumizi yanayotokana na Mfuko Mkuu chini ya Sheria ya Bunge:-

- (a) Afisa Mhasibu ana mamlaka ya kutumia fedha kadri ya sababu zilizobainishwa katika sheria; na
- (b) Mgawo wa fedha kwenye mafungu utazingatia utekelezaji, bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha.

Idhini ya  
kutumia fedha  
kutoka Mfuko  
Mkuu

**45.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwa mamlaka aliyopewa, atatoa idhini ya kutumia fedha za Mfuko Mkuu kwa Waziri.

- (a) Kiasi kinachotakiwa kulipwa katika miezi mitatu inayofuatia kwa ajili ya matumizi ya kisheria; na
- (b) Kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa huduma za mwaka wa fedha chini ya mamlaka ya Sheria ya Matumizi.

Utoaji wa  
malipo

**46.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali atalazimika, kwa hati itakayotolewa kwa mkono wake, kutoa idhini ya kufanya malipo kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Waziri-

- (a) Kiasi kinacho tarajiwa kulipwa katika kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya malipo ya matumizi ya Serikali; na
- (b) Kiasi kinachotarajiwa kulipwa kwa ajili ya kutoa huduma katika mwaka wa fedha kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Serikali.

Utoaji fedha  
kutoka Mfuko  
Mkuu

**47.** (1) Malipo hayatafanywa –

- (a) kutoka kwenye Mfuko Mkuu isipokuwa namna itakavyotolewa na sheria iliyoandikwa; na
  - (b) zaidi ya kiasi ambacho kimetolewa chini ya matumizi kwa huduma yoyote.
- (2) Kwa kuzingatia vipengele vya sheria inayohusiana na matumizi ya Serikali itatumika kuhusiana na utoaji wa fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu.

Malipo ya fedha kwa mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama

**48.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 23(1), Hazina italipa katika kila kipindi cha robo mwaka, kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwenda katika Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama, kama itakavyo kuwa, fedha zote zilizotolewa na Bunge kugharamia matumizi ya shughuli za Bunge na Mahakama kwa ajili ya robo mwaka huo.

Kibali cha Mhasibu Mkuu

**49.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa kibali alichonacho atawaidhinisha maafisa masuuli kufanya matumizi hadi kufikia kiwango kwa madhumuni na kwa kuzingatia masharti yaliyomo kwenye kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(2) Kibali hakitatolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali mpaka pale kiasi na makusudi ambayo yamesabisha kutolewa yamebainishwa katika kibali kilichotolewa na Mlipaji Mkuu.

(3) Kila kibali kitakachotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kitazingatia kiwango na masharti ambayo Waziri atayaainisha.

(4) Afisa Masuuli anaweza asifanye malipo yoyote au kukubali kulipa kutoka kwenye akaunti au kuingia miadi yoyote au matumizi, isipokuwa imeidhinishwa kwa kibali kufanya hivyo.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (4) “miadi” maana yake mkataba, makubaliano au mpangilio kwa ajili ya kufanya malipo.

Dhana ya miadi

**50.** Taasiri au Mashirika ya Umma itafanya miadi chini ya masharti yafuatayo-

- (a) Kiasi ambacho kitalipwa chini ya miadi ni sawa na au pungufu ya kiasi kilichopo kwa ajili ya matumizi;
- (b) Uhalali wa malipo yatakayofanywa chini ya miadi itakuwa imehakikiwa; na
- (c) Miadi ni kwa mujibu wa matoleo ya fedha ya bajeti ya robo mwaka.

Miadi ya miaka mingi

**51.**-(1) Miadi yoyote ya miaka kadhaa itahitaji kwanza kupata kibali cha Waziri.

(2) Kupata kwanza kibali cha Waziri kunahitajika kwa ajili ya kuhakikisha kuwa-

- (a) miadi haisababishi ukomo wa matumizi ya miaka kadhaa chini ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti;
- (b) kiasi ambacho kinatakiwa kulipwa chini ya miadi katika mwaka uliopo wa fedha kinatakiwa kiwe sawa au pungufu kuliko kiasi kilichopo kwa ajili ya matumizi;
- (c) uhalali wa malipo yatakayofanyika chini ya miadi ini budi yawe yamehakikiwa; na
- (d) sehemu ya miadi inayotakiwa kulipwa kwa mwaka husika wa bajeti ni sawa na robo ya bajeti iliyotolewa kama ipo.

Mfumo wa  
udhibiti wa  
miadi

- 52.**-(1) Serikali na Taasisi na Mashirika ya Umma yatahitajika-
- (a) kutunza mifumo ya udhibiti wa miadi ambapo miadi yote inayodhaniwa itaingizwa; na
  - (b) kuzuiwa malipo kufanyika kutoka kwenye bajeti bila ya miadi ya msingi kuwa imeingizwa kwenye mfumo wa udhibiti wa miadi na namba ya miadi kutolewa na mfumo.
- (2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (1), miadi yote ambayo haijatekelezwa itajumuishwa kwenye makadirio ya mwaka yakionesha-
- (a) kuna kiasi cha kutosha kwenye kipengele ili kikidhi miadi ya miaka kadhaa ambayo haijatekelezwa ambayo italipwa chini ya kipengele husika; na
  - (b) ukomo wa matumizi na maoteo ya kibajeti chini ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti yanaakisi kikamilifu miadi ya miaka kadhaa.

Mikataba ya  
Miradi ya  
Maendeleo

- 53.**-(1) Taasisi na Mashirika ya Umma yatakikiwa kwanza kupata kibali cha Waziri kabla ya kuingia kwenye mikataba yenye mahitaji ya kifedha.
- (2) Waziri anaweza, ndani ya siku thelathini, kutoa idhini ya kifedha kwa masharti kwamba mkataba unatimiza vigezo vya miadi ya miaka kadhaa na mradi unawezekana kwa maoni ya Waziri.

Taarifa za  
ndani za  
mwaka

**54.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali ndani ya muda uliobainishwa kwenye Kanuni atatakiwa, atawasilisha kwa Katibu Mkuu, taarifa ya Serikali na taasisi na mashirika ya umma kuhusiana na mapato na matumizi halisi kwa mwezi uliopita na kiasi ambacho kinatarajiwa kukusanywa au kutumika katika mwezi huo na Serikali.

(2) Taasisi na mashirika ya umma, mifuko maalum, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itatoa taarifa kwa Mlipaji Mkuu kuhusu mapato na matumizi katika kila robo mwaka.

(3) Kamishna wa Bajeti kwa kushirikiana na Kamishna wa uchambuzi wa sera, ndani ya muda utakaoelezwa na kanuni watachapisha taarifa utekelezaji wa bajeti ya robo mwaka.

(4) Maafisa Wahasibu, ndani ya muda utakaoelezwa kwenye kanuni atawasilisha taarifa ya utekelezaji ya robo mwaka kwa Katibu Mkuu Hazina.

Taarifa ya  
matumizi ya  
miadi

**55.**-(1) Afisa masuuli atalazimika kuandaa na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu taarifa ya robo mwaka ya miadi halisi na miadi ya makisio na hali ya kifedha ya kasma au mfuko, kutegemea shughuli za kasma au Mfuko na utekelezaji wa bajeti ya kasma ya Mfuko.

Taarifa za  
Utekezaji

**56.**-(1) Waziri, ndani ya miezi mitatu baada ya kuwasilisha bajeti kwenye Bunge na katika kila robo mwaka baada ya hapo atawasilisha kwenye Bunge, kwa mtiririko na kwa ujumla taarifa ya utekelezaji.

(2) Endapo Bunge halipo kwenye vikao vyake na katika tarehe zilizobainishwa kwenye kifungu kidogo (1), taarifa ya utekelezaji itawasilishwa katika Bunge katika siku ya pili, mara tu baada ya kuanza kwa Bunge.

(3) Taarifa ya Utekelezaji-

(a) itaonesha kipindi cha mapitio, na jinsi ambavyo malengo na shabaha katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti yamefikiwa; na

(b) kubainisha kiasi kifuatacho na kuvilinganisha na shabaha zinazoendana katika kipindi cha mapitio-

- (i) mapato halisi katika kipindi husika na ikilinganishwa wa matarajio;
  - (ii) matumizi halisi kwa fungu, yakitofautishwa baina ya matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa kipindi hicho; na
  - (iii) mikopo halisi kwa kipindi hicho, na kwa mwaka wa fedha hadi mwisho wa mwaka wa fedha.
- (4) Ambapo malengo na shabaha hayajafikiwa, taarifa ya kisheria itataja-
- (a) sababu za kwa nini malengo na shabaha hazikufikiwa;
  - (b) hatua za marekebisho zinachukuliwa kuhakikisha kuwa malengo na shabaha ambayo hayakufikiwa yatafikiwa katika robo ijayo; na
  - (c) Mapendekezo yoyote ya maamuzi ya kisera ya Serikali ambayo yanaweza kuathiri kwa kiwango kikubwa malengo na shabaha katika taarifa ya matarajio ya bajeti au utekelezaji wa kibajeti na kiuchumi kwa ujumla katika nchi.
- (5) Mhasibu Mkuu wa Serikali, ataandaa taarifa ya kila mwezi ya Mfuko Mkuu ambayo itahusisha mapato halisina ridhaa za matumizi zilizotolewa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu ili kutumika katika maandalizi ya taarifa mbalimbali.
- (6) Waziri atalazimika, ndani ya miezi sita baada ya Bunge kuidhiniha Bajeti ya mwaka na kila mwisho wa mwaka wa fedha, kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa ajili ya kujadiliwa.

Taarifa za  
Serikali za  
robo mwaka

**57.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali ataandaa taarifa ya mapato na matumizi halisi kwa ujumla wake ya Serikali na Taasisi na Mashirika ya Umma na kuwasilisha kwa Waziri ambaye atawasilisha kwenye Bunge mwezi mmoja baada ya mwisho wa kila robo mwaka.

(2) Afisa Masuuli ataandaa na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali taarifa za uhamisho wa fedha uliofanyika ndani ya Mafungu husika.

**SEHEMU VI  
USIMAMIZI WA MAPATO**

Misingi ya  
usimamizi  
wa mapato

- 58.-** Sehemu ya Mapato ya Bajeti itazingatia misingi ifuatayo-
- (a) mapato yote ya Serikali kutoka vyanzo vya ndani na nje yataingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina;
  - (b) yeyote aliyepewa mamlaka ya kukusanya mapato ya Serikali atawajibika katika ukusanyaji wa mapato wenye ufanisi, na utunzaji hesabu na utoaji taarifa kwa kuzingatia sheria husika na kuchukua tahadhari ili kuzuia ufujaji wa mapato ya Serikali;na
  - (c) mapato yote ya Serikali yataingizwa kwenye Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali.

Majukumu  
ya  
ukusanyaji  
mapato na  
usimamizi

**59.-(1)** Waziri ataweka utaratibu wa kupokea maoni na mapendekezo kuhusu makadirio ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha kutoka kwa Bunge ambayo yatawasilishwa kwa Waziri si zaidi ya tarehe 15 Februari.

(2) Majukumu ya Katibu Mkuu kuhusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatakuwa ni-

- (a) kusimamia na kuweka misingi ya mipango na utafiti wa vyanzo vya mapato vya sasa na fursa ya mapato zaidi zilizopo;
- (b) kuanzisha mfumo ambao utaweka muda maalum wa kupokea mapendekezo ya hatua za mapato;
- (c) kuandaa hatua za mapato kwa bajeti ya Serikali;
- (d) kutafuta rasilimali ikiwa pamoja na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kujumuisha fedha hizo kwenye michakato ya mipango, bajeti na utoaji taarifa na uwajibikaji kama inavyoelezwa na sheria hii.
- (e) kuboresha na kusimamia uwazi, ufanisi na namna inayofaa ya usimamizi wa mapato;



**SEHEMU YA SABA**  
**USIMAMIZI WA VIFUNGU VIDOGO VYA NJE YA MFUMO WA BAJETI YA**  
**SERIKALI**

Usimamizi  
wa kibajeti  
na kifedha za  
serikali za  
mitaa

**60.**-(1) Waziri atasimamia masuala ya kibajeti na kifedha ya mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), bajeti inayopendekezwa na bajeti zilizoidhinishwa kwa pamoja zitawasilishwa kwa Waziri kwenye dhamana ya mamlaka ya serikali za mitaa kwa kuzingatia muda maalum.

(3) Uanzishwaji na usimamizi wa asasi zinazofanya kazi nje ya mfumo wa bajeti na mifuko maalum ya serikali za mitaa kutahitaji idhini ya Waziri wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mamlaka ya  
Waziri  
kusamehe  
kodi, ada na  
tozo

**61.** Waziri anaweza kusamehe kodi, ada au tozo zilizowekwa na Serikali kwa mujibu wa vigezo kwenye sheria yoyote, ili mradi atatunza kumbukumbu ya kila msahama pamoja na sababu za kutoa msamaha husika na kutoa taarifa Bungeni katika kipindi cha kila robo mwaka.

Usimamizi  
wa kibajeti  
na kifedha na  
wa asasi  
nyingine za  
Serikali

**62.**-(1) Waziri mwenye dhamana usimamizi wa kibajeti na kifedha na asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko Maalum inayojumuishwa ndani ya Serikali Kuu na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) bajeti inayopendekezwa na bajeti iliyoidhinishwa ya asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko inatakiwa kuwasilishwa kwa Waziri na Waziri mwenye dhamana kwa kuzingatia muda maalum ulioelezwa kwenye Kanuni;

(b) mikopo kwa ajili ya asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko maalum itahitaji kupata kwanza kibali cha Waziri, endapo asasi hiyo iliyo nje ya mfumo wa bajeti ina uwezo huo kisheria.

SEHEMU YA NANE  
MASHARTI YA JUMLA

- Kanuni na maelekezo **63.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazohitajika kuwezesha utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.
- (2) Bila kuathiri masharti kifungu kidogo (1), kanuni zitakazotungwa zibaainisha-
- (a) yaliyomo na aina mbalimbali ya taarifa zinazohitajika na Sheria hii;
- (b) muda wa kufuata kuwasilisha taarifa kabla ya kuwasilisha Bungeni;
- (c) vigezo ambavyo Bunge litatumia kuamua endapo hoja za ukaguzi zimezingatiwa; na
- (d) kanuni au vigezo vitakavyotumika kubainisha mgao wa fungu haukuzingatia sheria hii.
- Kuongeza kipindi cha muda uliowekwa **64.** Bunge linaweza kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa au nyaraka zinazotakiwa kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Sheria hii au muda uliowekwa kikatiba kupitia azimio.
- Uwajibishaji wa mamlaka iliyoshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria **65.**-(1) Serikali na taasisi za umma zitakaposhindwa kutekeleza masharti ya Sheria hii, Waziri atalazimika kutoa maelezo na mazingira yaliyosababisha kushindwa kutekeleza masharti husika.
- (2) Endapo inapothibitika kwamba afisa wa umma kwa kusudia au kwa uzembe amesababisha Serikali au taasisi ya umma kushindwa kutekeleza masharti ya Sheria hii, Afisa huyo atakuwa ametenda kosa la kinidhamu na atachukuliwa hatua za kinidhamu na atawajibishwa yeye mwenyewe.
- (3) Waziri atachukua hatua za kurekebisha taasisi ya umma pale inaposhindwa kufuata taratibu za kifedha au matumizi za ziada au matumizi ambayo hayajaidhinishwa.
- (4) Hatua za kurekebisha zinazoainishwa katika kifungu kidogo cha (3) zitajumuisha:

- (a) kuwasilisha na kuidhinisha Mpango kazi;
- (b) kupunguza kiasi cha bajeti iliyotumika zaidi ya iliyoidhinishwa katika mwaka unaofuata wa fedha;
- (c) kuweka sharti la Waziri kuomba kibali kabla ya kufanya matumizi; na
- (d) kusitisha mamlaka ya Afisa Masuuli katika usimamizi wa fedha.

Hatua za urekebishaji dhidi ya Serikali na Taasisi za Umma

**66.**-(1) Waziri atachukua hatua za kurekebisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum ikiwemo Serikali, taasisi ya umma, pale Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum itakaposhindwa kufuata taratibu za kifedha au matatizo ya kifedha.

- (2) Hatua za kurekebisha zitajumuisha-
  - (a) Kuwasilisha Mpango wa Utekelezaji;
  - (b) Kuweka sharti la Waziri kuomba kibali kabla ya kufanya maamuzi;
  - (c) Kupunguza au kusimamisha uhamishaji wa fedha za bajeti; au
  - (d) Kuteua msimamizi wa fedha ambaye atakuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi.

Hatua dhidi taasisi za umma

**67.** Afisa wa umma aliyepo Serikalini, taasisi ya umma, Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum hatachukuliwa hatua mwenyewe za kiutawala au za makosa ya jinai kwa kufanya au kuacha kufanya kwa nia nzuri wakati wa utekelezaji au alipotakiwa kutekelezaji wajibu aliopewa au wakati wa utekelezaji wake wa majukumu aliopewa kwa mujibu wa Sheria hii na nafasi yake ya kazi.

Kuingia kwa dharura kwa mafias wa mamlaka

**68.** Sheria hii itakuwa na masharti ya mamlaka ya juu dhidi ya sheria nyingine katika masuala yoyote yanayohusu-

- (a) bajeti ya taifa, bajeti ya taasisi za umma, mamlaka za serikali za mitaa au wakala nje ya bajeti;

- (b) usimamizi wa mchakato wa bajeti;
- (c) utekelezaji, ufuatiliaji. Tathimini na utoaji wa taarifa wa bajeti;
- (d) usimamizi wa mapato na matumizi ya bajeti; na
- (e) kusimamia taasisi za umma na wakala nje ya bajeti.

Masharti ya  
Mpito

**69.**-(1) Sheria hii itakapoanza kutumika, fungu husika kwa ajili ya mafungu mbalimbali ambazo bado hazijawasilishwa kwa kuzingatia taarifa au utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi zitaanza kutumika siku baada ya makadirio kuwasilishwa Bungeni.

(2) Mafunguyataomba kiasi kinachotakiwa kwa ajili ya kukidhi matumizi muhimu ya shughuli za Serikali na taasisi za umma kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka huo.

(3) Bunge litaweka ukomo wa kiasi kitakachoidhinishwa kwa fungu husika kwa asilimia ishirini na tano au chini ya kiasi chote kilichopo katika makadirio ya mwaka endapo anayeomba vote hajatekeleza masharti ya kifungu cha 64.

(4) Katika kifungu hiki, “shughuli za Serikali” zitamaanisha huduma zozote zinazotolewa na kazi zinazofanywa na fungu ikiwa huduma hizo ni za kawaida au sio za kawaida.

**SEHEMU YA TISA**  
**MAREKEBISHO YATOKANAYO**  
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA BUNGE (UTAWALA)**  
**(SURA YA 115)**

Tafsiri  
Sura ya 115

**70.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Bunge (Utawala), ambapo itarejewa kama “Sheria kuu”.

Kuongezwa  
kwa kifungu  
cha 18A.

**71.** Sheria Kuu inafanyiwa marekebisho yafuatayo-

- (a) Kuongeza kifungu kipya cha 18A. mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

“Kuanzishwa  
kwa Ofisi ya  
Bunge ya  
Bajeti

18.A (1) Kutakuwa na Ofisi ya Bunge ya Bajeti ndani ya huduma za Bunge, ambayo itakuwa na watumishi watakaoteuliwa na Tume ya Huduma za Bunge kwa kuzingatia ujuzi, kuanzishwa kwa Ofisi ya Bunge utaalumu na uzoefu katika masuala ya fedha, uchumi na sera za umma.

(2) Ofisi ya Bunge ya Bajeti itafanya uchambuzi wa kina na kwa wakati kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati zake.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu kidogo cha (2), Ofisi ya Bunge ya Bajeti itatekeleza yafuatayo:

- (a) kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu taarifa zinazohusu bajeti, fedha na kiuchumi kwa Kamati za Kudumu za Bunge;
- (b) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Bunge na Kamati zake za kudumu katika kutekeleza majukumu yake;
- (c) kuliwezesha Bunge kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii;
- (d) kuandaa taarifa kuhusu maoteo na mapendekezo ya masuala ya kibajeti kwa Bunge na Kamati zake za Kudumu;
- (e) kutoa taarifa zinazohusu Bajeti kwa Kamati za Kudumu za Bunge katika maeneo yao ya kiutawala;
- (f) kuwasilisha taarifa kuhusu maoteo ya kiuchumi, maoteo ya kibajeti na jinsi ya kupunguza nakisi ya bajeti.

- 
- (g) kubainisha na kutoa mapendekezo kuhusu Miswada ya Sheria na hati za kisheria ambazo zinahusu ongezeko au punguzo la mapato na bajeti ya Serikali;
  - (h) kuandaa tafiti kuhusu masuala mahsus kama vile vihatiarishi vya kifedha vinavyosababishwa na mMashirika na taasisi za umma na pia masuala ya sera ya fedha;
  - (i) kutoa ushauri wa jumla kwa Bunge na Kamati zake za Kudumu za Bunge kuhusu bajeti ya Serikali na uchumi wa Taifa;
  - (j) kuandaa uchambuzi wa masuala mahsusi, pamoja na vihatiarishi vya kifedha vinavyosababishwa na Serikali na sera za Serikali na shughuli zake na kushauri Bunge na Kamati zake za Kudumu;
  - (k) kupitia mapendekezo ya Bajeti ya Serikali na mwelekeo wa uchumi na kulishauri Bunge;
  - (l) kuanzisha na kukuza uhusiano na HAZINA na asasi nyingine ya kitaifa na kimataifa maslahi katika masuala ya Bajeti na masuala ya Kijamii na Kiuchumi kama ambavyo itaona zinafaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi;
  - (m) kuhakikisha taarifa na nyaraka nyinginezo zinazoandaliwa na Ofisi ya Bunge ya Bajeti zinaandaliwa, kuchapidhwa na kusamazwa;

- (n) kutoa taarifa kwa Kamati za Bunge za Kudumu kuhusu Muswada wowote wa Sheria uliowasilishwa Bungeni ambao unahusu masuala ya kiuchumi na kifedha, kwa kufanya reja kwenye misingi ya kibajeti na malengo ya kifedha yaliyobainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajet; na
- (o) kupendekeza kwa kamati ya Bunge ya Bajeti mfumo mbadala wa mapato kwa mwaka husika wa fedha.
- (4) Katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Bunge ya Bajeti itazingatia misingi ya kushirikisha Umma katika masuala ya kibajeti.”;
- (b) kufuta vifungu vya 28na 29 na kuweka badala yake yafuatavyo:
- “Makadirio na mapato 29.-(1) Katibu ataandaa kila mwaka, makadirio ya mapato na matumizi ya Bunge na kuyasafirisha kwenye Tume ya Huduma za Bunge kwa mapitio na kuridhia.
- (2) Katibu atawasilisha kwenye kikao cha mashauriano kitakacho jumuisha Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango na kamati ya Bunge ya Bajeti madadirio yaliyoidhinishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa kupitishwa.
- (3) Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atawasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Bunge kwa kuidhinishwa.”; na

- (c) kurekebisha vifungu vya 31 hadi 41 ili visomeke kama vifungu vya 30 hadi 40

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKAGUZI YA UMMA  
(SURA YA 418)**

Tafsiri

**72.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma hapa ikirejewa kama “Sheria kuu”.

Marekebisho  
ya kifungu cha  
44

**73.** Sheria kuu irekebishwe kwenye sehemu 44(2), kwa kufuta maneno “Kamati ya Hesabu za Serikali marekebisho ya kifungu cha 44 na badala yake kuweka maeneo “Kamati ya Bunge ya Bajeti”.

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTAWALA WA MAHAKAMA  
(SURA YA 237)**

Tafsiri

**74.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utawala wa Mahakama ambapo itarejewa kama Tafsiri “Sheria kuu”.

Marekebisho  
ya kifungu cha  
44

**75.** Sheria kuu inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 59 na kuandika kifungu kipya kifuatacho:

“Makadirio  
ya mapato na  
matumizi ya  
Mahakama

**59.-(1)** Mtawala Mkuu wa Mahakama, kila mwaka wa fedha ataandaa makadirio ya mapato na matumizi ya mahakama na kuyawasilisha kwenye Tume kwa mapito na kuridhiwa.

(2) Mtawala Mkuu wa Mahakama atawasilisha makadirio yaliyoridhiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa Kamati ya Bunge ya bajeti kwa kujadiliwa na kupitishwa kwenye kikao cha mashauriano kati ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha, Waziri mwenye chamana ya masuala ya mipango.



(3) Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atawasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya mahakama kwa ajili ya kupitishwa. ”

Imepitishwa na Bunge tarehe 28 Machi, 2015

THOMAS D. KASHILILLA  
Katibu wa Bunge